# Barazani

Jarida la **Baraza la Habari Tanzania**
Toleo la **187, Julai, 2024**
ISSN **0856-874X**

*Kukuza Uhuru wa Vyombo vya Habari na kuhakikisha viwango vya juu kabisa vya weledi na uwajibikaji*



# Usawa, Haki katika Uchaguzi Msingi wa Demokrasia


## Tasnia yaomboleza kifo cha Jaji Mlay UK 6

**Kilele cha EJAT Septemba 28** Uk 8

**MCT na mabadiliko** Uk 12

**Sheria ya habari Zanzibar** Uk 20

# Vyama vya Siasa vipewe nafasi sawa habari za uchaguzi




Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Joseph Warioba akizungumza katika Kongamano la Wadau kuhusu Wajibu wa Vyombo vya Habari Kuhakikisha Uchaguzi wa Kuaminika lilioandaliwa na Baraza la Habari Tanzania Aprili 30, JijiniDodoma.

**MCT, MSHINDI WA TUZO YA IPI 2003 FREE MEDIA PIONEER**



Watanzania wanakabiliwa na jukumu muhimu la kuchagua viongozi wa serikali za mitaa na Rais, wabunge na madiwani kwenye hii miaka miwili.

Ifikapo Novemba 27,2024 wananchi wa Tanzania watachagua viongozi wa serikali za mitaa wakati mwakani uchaguzi mkuu utafanyika kuchagua Rais, wabunge na madiwani.

Uchaguzi ni msingi muhimu wa demokrasia kwa kuwawezesha wananchi kuchagua wawakilishi wao na kushiriki katika utawala hasa nyakati hizi ambapo kuna vyama vingi vya siasa jambo ambalo huchangia kuleta shauku kubwa kwa wananchi na wanasiasa kila zinapofanyika.

Wadau mbalimbali kupitia vyombo vya Habari wana jukumu la kuelimisha umma kuhusu masuala ya uchaguzi ili kuwapa wananchi elimu sahihi ya kushiriki zoezi zima la upigaji kura kwa ngazi zote na upatikanaji wa matokeo. Hii itasaidia kupunguza/kuondoa dhana iliyojengeka ya changamoto za wizi wa kura, rushwa na hata ujanja wa kubadilisha matokeo, lakini pia kuchagiza kuwepo umakini na ulinzi wa kura za wananchi.

Kwa vyombo vya habari, wakati wa uchaguzi vinakabiliwa na changamoto na huhitajika umakini na dhamira ya ziada katika kuhudumia wananchi kuhakikisha kuwa ni wale tu wanaostahili na wenye sifa ndio wanachaguliwa.

Baraza la Habari Tanzania (MCT) taasisi yenye jukumu la kuhakikisha vyombo vya habari vinazingatia maadili na weledi limedhamiria kusaidia vyombo vya habari kukabiliana na changamoto za uchaguzi.

Baraza kwa mwelekeo wake wa mabadiliko limeandaa mpango wa kitaifa wa utekelezaji ambao utasaidia vyombo vya habari kutimiza majukumu yao na kuhakikisha uchaguzi wa kuaminika.

Kwa kutambua udhaifu wa vyombo vya habari katika maandalizi ya pamoja, kushughulikia masuala yasiyo muhimu badala ya masuala yatakayo wawezesha wananchi kufanya maamuzi muhimu wakati wa kupiga kura, Baraza litashughulikia changamoto hizo kwa kuchukua hatua za maandalizi, kuwezesha vyombo vya habari kufichua makosa na kuanzisha mijadala ya kujenga taifa.

Sasa ni muhimu kwa vyombo vya habari kusimama imara kuhakikisha kuwa chaguzi zinakuwa za mafanikio na masuala ya rushwa , wizi wa kura na matatizo mengine yanakuwa historia.

Hivyo ni muhimu kwa vyombo vya bahari kukuza na kudumisha ushirikiano na mipango ya pamoja ili kufanikisha na kufikia malengo ya kuwa na uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika utakaotoa nafasi sawa kwa vyama vya siasa kuhusiana na habari za uchaguzi

**BODI YA UHARIRI:**
Ernest Sungura Katibu Mtendaji – MCT
Hamis Mzee Mhariri

**MAWASILIANO**
Kwa Maoni na Malalamiko:
Katibu Mtendaji
Baraza la Habari Tanzani (MCT)
S.L.P. 10160, Dar es Salaam
Simu: +255 22 27775728, 22 2771947
Simu ya Kiganjani: +255 784 314880
Fax: + +255 22 2700370
Baruapepe: media@mct.or.tz
Tovuti: www.mct.or.tz
Facebook:- www.facebook.com/mediacounciltanzania Twiter:- www.twitter.com/mctanzania




Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Jaji Joseph Warioba (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Kongamano la Wadau kuhusu Wajibu wa Vyombo vya Habari Kuhakikisha Uchaguzi wa Kuaminika ulioandaliwa na Baraza la Habari Tanzania uliofanyika Dodoma.

# Usawa, Haki katika Uchaguzi Msingi wa Demokrasia

**Na Mwandishi wa Barazani**

Washiriki wa Kongamano la wadau wa habari na uchaguzi lililoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) wamejadili pamoja na mambo mengine umuhimu wa usawa, haki na uwajibikaji kwa viongozi wa siasa, umma na vyombo vya habari kuwa ndiyo msingi wa demokrasia nchini.

Kongamano hilo lilifanyika Jijini Dodoma, Aprili 30, mwaka huu, mgeni rasmi akiwa ni Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mstaafu, Jaji mstaafu Joseph Sinde Warioba.

Kauli mbiu ya kongamano hilo ilikuwa ni Uandishi wa Habari za Uchaguzi kwa weledi hujenga Usawa, Haki na Uwajibikaji.

Akifungua mkutano huo wa wadau, Jaji Warioba, alisema katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi hujitokeza changamoto mbalimbali maandalizi dhaifu ya vituo vya kupigia kura, kasoro za usambazaji vifaa vya kupigia kura, rushwa wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama, uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo ya kura.

Jaji Warioba alisema kuwa ni muhimu kushughulikia changamoto hizi kwa kuwa kuzipuuza siyo tu kunakwaza demokrasi bali kunyima fursa ya kupiga kura kwa wananchi na kusababisha vurugu katika jamii.

Alivitaka vyombo vya habari vizingatie kutenda haki, usawa na kuwajibika ili kuhakikisha uchaguzi huru na wa haki kwa kuwaelimisha wananchi kwa kufanya utafiti na kuangalia masuala yanayoathiri wananchi badala ya matukio.

'Vyombo vya habari vitoe kipaumbele katika kuridhisha wananchi badala ya manufaa ya vyama vya siasa, viripoti kwa kutegemea utafiti, na kuepusha kujirudia kwa changamoto katika chaguzi kwa kuchukua hatua mapema," alisema Jaji Warioba.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania,Ndugu Ernest Sungura, mapema alisema katika kongamano hilo kwamba baraza limeandaa mpango wa kitaifa unaolenga kuviwezesha vyombo vya habari kutimiza wajibu wake kwa ufanisi katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi unaokuja wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Moja ya maeneo ambayo Ndugu Sungura alisisitiza ni uandishi wa uchaguzi uliolenga kuwapatia wananchi taarifa sahihi, zisizoegemea upande wowote na zinazozingatia maadili ya uandishi wa habari kwani kwa kufanya hivyo alisema kutajenga imani ya umma, kukuza haki katika michakato ya uchaguzi na uhalali wa matokeo ya uchaguzi.

Alisema vyombo vya habari vina wajibu wa kuongeza elimu kwa

*Endelea Ukurasa wa 4*

# Usawa, Haki katika Uchaguzi Msingi wa Demokrasia

*Inatoka Ukurasa wa 3*

mpiga kura ili kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi kwenye sanduku la kura.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema dhamira ya pamoja katika kujenga sekta ya uandishi habari imara na uwajibikaji, hasa kuelekea chaguzi zijazo ni muhimu kwa kuwa wajibu wa vyombo vya habari katika demokrasia ni muhimu katika kuelimisha na kuwezesha midahalo miongoni mwa wananchi hasa kipindi cha uchaguzi.

Alisema ni muhimu kwamba vyombo vya habari vinakuwa na viwango vya juu vya weledi, vikizingatia maadili na kukuza uandishi wa uwajibikaji kukabiliana na upotoshaji wa taarifa na taarifa chonganishi ambazo zinaweza kukwaza wananchi wakati wa uchaguzi.

Serikali, alisema, imedhamiria kuhakikisha uhuru wa habari wakati inahakikisha uwajibikaji na kuendesha uchaguzi jumuishi na wa wazi na kuongeza kuwa kuna haja ya ushrikiano kuleta mazingira wezeshi kwa vyombo vya habari kufanyakazi kwa uhuru bila woga wala vitisho.

Aliwataka wadau kujadiliana kwa uwazi kwa lengo la kuimarisha uwezo wa vyombo vya habari kutoa habari sahihi katika mchakato wote wa uchaguzi, na kusisitiza umuhimu wa kushirikiana katika kuboresha uandishi wa habari za uchaguzi na kujenga kujiamini katika mchakato wa uchaguzi.

Akizungumza katika mkutano huo wa wadau, Katibu wa Uenezi, Itikadi na Mafunzo wa CCM ,



*Zitto Kabwe Mwanasiasa wa chama cha ACT Wazalendo akiwa katika mkutano huo.*



*Aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi akizungumza katika mkutano huo.*

Amos Makalla, alisema kuwa CCM itaongoza katika utekelezaji wa haki, usawa na uwajibikaji kwa kuhakikisha uchaguzi wa haki na huru. Ndugu Makala alikuwa akimwakilisha Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi.

Wengine waliohudhuria katika mkutano huo wakiwa katika jopo lililoratibiwa na Rosemary Mwakitwange, mshauri wa habari yaliwajumuisha Moses Kimaro, Mkurugenzi wa Utafiti na Maendeleo wa Taasisi ya Wajibu , Mhandisi Andrew Kisaka – Mhandisi Mkuu Utangazaji Mamlaka ya Udhibiti ya Mawasiliano Tanzania(TCRA), Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Hamad Masoum , Zitto Kabwe wa chama cha ACT – Wazalendo na David Misiime – Naibu kamishna wa Polisi.

Jopo lingine lililoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications, Bakari Machumu liliwajumuisha waandishi wa habari wakongwe Jenerali Ulimwengu, Edda Sanga na Pili Mtambalike na Mkurugenzi wa Jamii Forums, Maxence Mello.

Moja ya mambo ambayo yaliibuliwa na wanajopo ni pamoja na kuvihimiza vyombo vya kusimamia sheria kuhakikisha vinadumisha amani na kuwalinda waandishi wa habari wakati wa uchaguzi ili kujenga misingi ya vyombo vya habari kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa au kutishwa.

Aidha, katika kongamano hilo uzoefu wa nchi nyingine katika chaguzi ulielezwa na Jacob Nyukuri Nyongesa, Ofisa mwandamizi wa Utafiti, Mipango na Mikakati wa Baraza la Habari la Kenya (MCK) na Dk. Jennifer Thomas, Profesa Mshiriki , Idara ya Habari,Uandishi na Filamu ya Chuo Kikuu cha Howard cha Marekani.

Nyongesa alisema ingawa uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu kwa utawala wa kidemokrasia lakini licha ya kupiga hatua, changamoto bado zipo na kwamb a ni muhimu kuendelea kuheshimu haki ya uandishi, kukabiliana na habari potofu na kulinda michakato ya demeokrasia.

Kwa upande wa Marekani, Dk. Jennifer alisema uzoefu wa nchi hiyo unathibitisha umuhimu wa uandishi wa habari katika michakato ya demokrasia.

"Licha ya changamoto kama uandishi wa upendeleo na kushuka kuaminika, waandishi wa habari wanabaki kuwa muhimu kwa kuwawajibisha wenye mamlaka na kuupasha habari umma", alisema na kuongeza kuwa kukua kwa dhamira na uandishi wa kuzingatia maadili na kuzingatia

*Endelea Ukurasa wa 10*



Rehema Kongola, Meneja mpya wa Fedha na Utawala wa MCT.



Ziada Kilobo, Meneja wa ofisi ya MCT Zanzibar.



Elizabeth Okuli, Ofisa wa Raslimali watu na Utawala.

# MCT katika mabadiliko

**Na Josephat Mwanzi**

Baraza la Habari Tanzania (MCT) limeanzisha mchakato wa mabadiliko chini ya uongozi wa Katibu Mtendaji mpya, Ernest Sungura.

Akihitimisha siku 100 ofisini, Sungura ametangaza mabadiliko kwa timu ya utendaji, kuhamasisha ari mpya, kasi na nguvu katika Baraza.

"Hatufanyi mabadiliko tu, tunaanza hatua za kuleta mapinduzi katika sekta ya habari Tanzania. Lengo letu ni kuimarisha utendaji wa Baraza na kuleta tija zaidi," Sungura alisema katika mkutano na wafanyakazi wa Baraza Mei 14, 2024.

Katika mabadiliko ya kimuundo ya Baraza, Rehema Kongola, Mhasibu mwenye CPA ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), ameteuliwa Meneja mpya wa Fedha na Utawala.

"Uzoefu wa Kongola utakuwa muhimu katika kusimamia masuala yetu ya fedha na uchambuzi," amesema Sungura.

Ziada Kilobo aliyekuwa Meneja wa Rasilimali Watu na Utawala amepewa jukumu la kusimamia uendelevu na pia kuongoza Ofisi ya MCT, Zanzibar.

Pia amepewa jukumu la kusimamia kitengo cha ushauri ambacho Sungura amesema ni njia ya aina yake ya kutafuta mapato kwa lengo la kujenga uendelevu kitaasisi.

Elizabeth Okuli amepandishwa kutoka nafasi ya Katibu Msaidizi katika ofisi ya Katibu Mtendaji na Ofisa Utawala Msaidizi na kuwa Ofisa Rasilimali Watu, Utawala na manunuzi.

"Kujitoa kwa dhati na utendaji wa kazi wa Okuli kumewezesha kupandishwa cheo alichostahili," alisema Sungura.

Mabadiliko haya yamekuja baada ya Sungura kuhitimisha kwa mafanikio siku 100 akiwa ofisini ambapo aliongoza Baraza kuandaa mkutano muhimu uliolenga kwenye wajibu wa kuripoti na kutangaza uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2024 na uchaguzi mkuu mwakani.

Mkutano huo ulioandaaliwa na MCT uliwakutanisha wanahabari, wanasiasa na wanazuoni jijini Dodoma, Aprili 30, 2024.

"Tunaanzisha zama mpya za ubunifu, ukuaji na dhamira ya dhati kuboresha misingi ya uandishi wa habari ," Sungura amesema

Hata hivyo amesema mwelekeo wa mabadiliko unakabiliwa na changamoto kubwa ikiwemo uwezo wa kujitosheleza wa vyombo vya habari.

Kushinda vikwazo hivi, Sungura alisema anahimiza wadau na wahisani kuunga mkono jitihada za kuimarisha tasnia ya habari.

# Tasnia ya habari yaomboleza kifo Jaji Mlay

Na Mwandishi wa Barazani

Kwa Baraza la Habari Tanzania (MCT) na jumuia ya wanahabari kwa jumla Mei 25, 2024 ilikuwa ni siku ya huzuni kutokana na kufariki kwa Jaji Mstaafu Juxon Mlay.

Jaji Mlay alikuwa akitumikia kipindi cha pili akiwa Rais wa Baraza la Habari na pia Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza.

Alichaguliwa kwa mara ya pili Septemba 2023 katika Mkutano Mkuu wa Baraza uliofanyika Arusha.

Hayati Mlay aliuendesha mkutano huo kwa njia ya mtandao akiwa India ambako alikwenda kwa matibabu.

Hii ilikuwa mara ya pili kwake kuongoza Mkutano Mkuu wa Baraza unaofanyika kila mwaka mara moja kwa njia ya mtandao akiwa India ambapo alikwenda mara tatu kwa matibabu.

Bahati mbaya, katika mara hii ya tatu akiwa India Jaji huyo aliyeheshimika kwa kusimamia kanuni na mahiri, alifariki.

Kabla ya kuwa Rais, Jaji Mlay alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Maadili la Baraza kwa kipindi cha miaka sita.

Jaji Mlay atakumbukwa kwa uthabiti wa kusimamia haki na kuhakikisha kanuni za haki zinazingatiwa na vyombo vya habari na wanahabari.

Kama Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, hayati Jaji Mlay alisisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili, kanuni na taratibu za tasnia ya habari ili viendeshwe kwa weledi.

Alivitembelea vyombo vya habari vilivyokuwa na changamoto za kimaadili na kuvishauri njia nzuri ya kukabiliana nazo.

Jaji Mlay aliyekuwa Jaji aliyeheshimika alihudumu kwenye Mahakama Kuu na mapema aliwahi kuwa Mwandishi wa Sheria wa Bunge na Mkurugenzi wa Mashitaka.

Alichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa mjumbe wa Bodi ya MCT mwaka 2014, ambako alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kutoka mwaka huo hadi 2017 na alichaguliwa tena Septemba 29, 2017. Pia alikuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi ya Baraza.

Kutoka 1977 hadi 1981, alikuwa Mwandishi wa Sheria Msaidizi na baadaye kutoka 1981 hadi 1986, alihamishiwa katika Taasisi ya Kuzuia na Kukabiliana na Rushwa ambako alikuwa Mkuu wa Idara ya Kuendesha Mashtaka.

Kutoka 1987 hadi 1989, alipandishwa kutoka Msaidizi Mwandamizi wa Mwandishi wa Sheria.

Jaji Mlay pia alihamishiwa katika Sektretariati ya Bunge kati ya mwaka 1989 na 1991 na aliteuliwa kuwa Msaidizi Mwandamizi wa Katibu wa Bunge. Kutoka 1991 hadi 1993, aliteuliwa kuwa Naibu Mwandishi wa Sheria.

Kati ya 1993 na 1997, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa kwanza wa Masuala ya Katiba katika Wizara ya Sheria na Masuala ya Katiba na kutoka mwaka 1997 hadi 2000, aliteuliwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kutokana na umahiri wake, Jaji Mlay aliteuliwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania mwaka 2000, wadhifa alioendelea nao hadi 2009.

Katika sala ya mazishi yake iliyofanyika katika Kanisa la Azania Front Jijini Dar es Salaam,wakuu wa taasisi za kihabari nne - Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania(TEF), Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania(TAMWA) Joyce Shebe na Rais wa Umoja wa Klabu za Waandishi Tanzania (UTPC) Deogratius Nsokolo walieleza msimamo ulioshabihiana kuhusu pigo kwa tasnia ya habari kutokana na kifo cha Jaji Mlay.

Wote walimwelezea Jaji Mlay kuwa alikuwa mahiri na thabiti katika kusimamia haki, maadili na weledi katika vyombo vya habari.

Sungura pia alisema ,kifo cha Jaji Mlay (74) kilikuwa ni pigo kubwa kwa Baraza.

Katika maelezo yake kuhusu uongozi thabiti wa Jaji Mlay,Sungura aliwaeleza waombolezeaji wakiwemo wajumbe wawili wa Bodi ya Udhamini ya MCT – Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza mstaafu, Jaji Joseph Warioba na Profesa Geofrey Mmari na Rais wa MCT na Mwenyekiti wa Bodi alieyemtangulia, Jaji Thomas Mihayo kuwa hayati Mlay alisimamia mchakato uliofanikisha uteuzi wake kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza.

Uteuzi wa Sungura uliofanywa na Bodi ya MCT ulitangazwa na Jaji Mlay katika Mkutano Mkuu uliofanyika Arusha.

Jaji Mlay ambaye ameacha mjane na mabinti wawili alizikwa Mei 31, 2024 ,Moshi,Mkoani Kilimanjaro.



*Hayati Jaji mstaafu Juxon Mlay, Rais wa MCT na Mwenyekiti wa Bodi.*



Rais Dk.Samia Suluhu Hassan akihutubia katika Kongamano la Kitaifa la Maendeleo ya Sekta ya Habari Jijini Dar es Salaam.

# Vyombo vya habari washirika muhimu wa maendeleo – Samia

Na Saumu Mwalimu

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amehakikisha kuwa vyombo vya habari sio adui bali ni washirika muhimu wa maendeleo.

Katika hotuba yake ya ufunguzi katika Kongamano la pili la Kitaifa la Maendeleo ya Sekta ya Habari lililofanyika Juni 18 hadi 19, 2024, alisisitiza dhamira yake kwa uhuru wa kujieleza.

Aliwaaambia washiriki zaidi ya 1,200 wa kongamano hilo Jijini Dar es Salaam kuwa ni ruhsa kwa wenye mtazamo kinzani kutoa maoni yao lakini akatahadharisha maoni hayo kinzani yasiathiri hadhi za wengine na kusababisha maumivu.

Kongamano hilo lililoandaliwa kwa ushirikiano baina ya Umoja wa Kutetea Haki ya Kupata Taarifa (CoRI) na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, limesisitiza wajibu muhimu wa vyombo vya habari katika kukuza uhuru wa kujieleza na kuwepo mazingira wezeshi kwa maendeleo.

Rais Samia alisisitiza kwamba wajibu wa serikali ni kuweka mifumo, sheria na kanuni kuhakikisha mazingira salama na wezeshi kwa vyombo vya habari kufanyakazi.

"Hii ni kwa sababu vyombo habari siyo adui bali mshirika muhimu wa maendeleo ya nchi yetu ," alisisitiza.

Rais amehimiza vyombo vya habari kutumia fursa ya uhuru wa kujieleza iliyopo kwa umakini na kusisitiza "serikali itatimiza wajibu wake, na nyie mtimize wenu".

Rais alieleza wasiwasi kuhusu kasi ndogo ya vyombo vya habari kutumia maendeleo ya teknolojia

Endelea Ukurasa wa 10



*Washindi wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) mwaka 2022 wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni wa heshima wa tuzo hizo, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Ombeni Sefue (wanne kutoka kushoto mstari wa mbele na viongozi wengine) katika kilele cha tuzo hizo kwenye ukumbi wa Mlimani City.*

# Kilele cha EJAT Septemba 28

**Na Mwandishi wetu**

Baraza la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na washirika wake ambao ni wadau na taasisi za kihabari linaandaa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2023 ambazo kilele chake kitakuwa Septemba 28, 2024 jijini Dar es Salaam.

Tuzo hizo ambazo zitakuwa zinafanyika kwa mara ya 15 mfululizo toka zilipoanzishwa mwaka 2009, zimepokea jumla ya kazi 1,069 kwa mwaka 2023 hiki kikiwa kiwango cha juu kuwahi kutokea.


Tuzo hizo ambazo zimekuwa kivutio kikubwa kwa waandishi wa habari nchini Tanzania, zinatarajiwa kuhudhuriwa na watu 350 ambao ni waandishi wa habari, wadau wa habari, viongozi kutoka serikalini, wadau wa maendeleo pamoja wakufunzi wa vyuo vikuu.

Kwa mara ya kwanza Tuzo zitahusisha kazi ambazo hazikuwasilishwa na waandishi kwenye mashindano hayo. Kazi hizo ni zile ambazo zimeletwa kupitia jopo la wataalam ambao waliteuliwa kufanya kazi ya kutafuta habari ambazo zilihusu mkataba wa DP World, janga la Hanang na mgogoro wa Ngorongoro.

Habari katika maeneo hayo zitawasilishwa kwa majaji watakaopitia kazi zilizowasilishwa na waandishi kwa utaratibu wa zamani na kutoa wateule ambapo, washindi watatangazwa siku ya Tuzo, Septemba 28, 2024.



*Baadhi ya wawakilishi wa wadhamini Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT) 2022 wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Ombeni Sifue (katikati) katika kilele cha tuzo hizo.*




*Waziri Mkuu wa zamani na Makamu wa Kwanza wa Rais, Joseph Warioba (wa pili kutoka kushoto) akiwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura (kushoto) Mjumbe wa Bodi ya MCT, Joyce Bazira ( wa pili kulia) na Katibu Mtendaji mstaafu wa MCT, Kajubi Mukajanga wakionyesha Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari nchini ya mwaka 22/23 katika uzinduzi wake.*

# Vyuo vyahimizwa kuzingatia ubora taaluma

**Na Tumbi Kiganja**

Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari Tanzania 2022-2023, imezinduliwa Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa tasnia ya habari nchini.

Moja ya mambo ambayo yalibainishwa na Mtafiti Kiongozi wa ripoti hiyo, Dk. Samwilu Mwaffisi ni kuwa taasisi nyingi za uandishi wa habari zinaweka kipaumbele cha wingi wa wanafunzi kuliko ubora wa elimu wanayoitoa.

Dk. Mwaffisi ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Tumaini, alisema hayo Julai 4, 2024 wakati wa uzinduzi wa Ripoti hiyo iliyozinduliwa Jijini Dar es Salaam na Waziri Mkuu wa zamani na Makamu wa Kwanza wa Rais, Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba.

Alisema kutokana na hali hiyo mara nyingi wahitimu huondoka wakiwa na alama za juu lakini ujuzi wa kiutendaji usiotosheleza katika tasnia hiyo, hivyo kuibua changamoto kubwa katika elimu ya uandishi wa habari na uhuru wa vyombo vya habari.

Ripoti hiyo iliibua masuala kadhaa, ikiangazia wazi kero za wadau wa habari kuhusu ubora wa wahitimu kutoka taasisi za sasa za uandishi wa habari.

Alibainisha kuwa bidhaa za mwisho za taasisi hizo mara nyingi huwa hazijaandaliwa vizuri hivyo hupata changamoto kupenya kwenye soko la ajira.

"Wahariri, kwa mfano, waliripoti kwamba wanahabari wengi wachanga hawana ujuzi wa kimsingi, kama vile kuandika aya ya utangulizi ya habari, na kuwalazimisha wahariri hao kuchukua jukumu la kufundisha upya jinsi ya kuandika habari,". alisema.

Dk. Mwaffisi alipendekeza kuwa ni wakati muafaka kwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), MCT, wamiliki wa vyombo vya habari, taasisi za uandishi wa habari na Baraza la Taifa la Elimu na

*Endelea Ukurasa wa 14*

# Vyombo vya habari washirika muhimu wa maendeleo – Samia

*Inatoka Ukurasa wa 7*

huku akitahadharisha haja ya kuwa makini kuepukana na mwenendo wa uandishi wa mtandaoni.

"Ingawa ni muhimu kwa sekta ya habari kwenda sawia na mabadiliko ya teknolojia, ni muhimu tujikumbushe kwamba kalamu ni hatari zaidi kuliko upanga. Kwa vile athari inayosababishwa na habari moja inaweza kuwa kubwa, ni muhimu kwamba uhuru na maendeleo ya habari za mtandaoni utumiwe kwa makini", aliongeza.

Rais Samia pia amesisitiza haja ya waandishi kuandika habari za uchambuzi kwa kuwa habari nyingi ni za kuripoti matukio.

"Pia andikeni habari za manufaa kwa umma hata kama hazitawafanya kuwa maarufu," alisisitiza.

Kauli mbiu ya kongamano hilo lililohudhuriwa na wahariri, maofisa wa mawasiliano wa serikalni, wasomi na wasimamizi wa vyombo vya habari ni " Kuzipa nguvu kauli, kuboresha mielekeo, kujenga na kuimarisha uendelevu kwa sekta ya habari katika zama za Kidijiti".



*Baadhi ya washiriki wa kongamano la kitaifa la maendeleo ya sekta ya habari nchini wakifuatilia kwa makini yanayoendelea kwenye kongamano hilo.*

# Usawa, Haki katika Uchaguzi Msingi wa Demokrasia

*Inatoka Ukurasa wa 4*

uhuru wa habari ni muhimu katika kuheshimu haki ya mfumo wa uchaguzi na tunu za demokrasia.

Wakichangia katika mada mbalimbali katika kongamano hilo, wadau walisisitiza umuhimu wa kutoa nafasi sawa kwa vyama vya siasa wakati wa uchaguzi na kukabiliana na nguvu ya wanasiasa ambao siku zote hutaka upendeleo kwa kuwanunua waandishi wa habari.

Katika kongamano lingine lililofanyika Juni 18 na 19, mwaka huu Jijini Dar es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiwa ni mgeni rasmi aliwatahadharisha waandishi wa habari kutumia kalamu zao kujenga na siyo kubomoa.

Alisema vyombo vya habari vifanye uchambuzi wa yanayofanywa na vyama vya siasa ili wachukue hatua za kuboresha utendaji wao na kwamba wawaelimishe wananchi kuhusu wajibu wao na haki ya kupiga kura.

Kongamano la wadau wa habari na uchaguzi limeandaliwa kwa ufadhili wa Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania kufuatia kuwepo kwa uchaguzi wa serikali za mitaa ambapo watanzania wanatarajia kupiga kura ya viongozi wa serikali za mitaa Novemba 27, mwaka huu na kushiriki kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

# Sungura atembelea viwanja, shamba la MCT

Na Mwandishi wa Barazani

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura ametembelea mali za Baraza hilo vikiwemo viwanja 19 na shamba wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, Februari 8, 2024.

Sungura amefanya ziara hiyo ikiwa ni sehemu ya kuzijua rasilimali za Baraza hasa ikizingatiwa kuwa yeye ni kiongozi mpya wa chombo hicho kikubwa nchini kinachosimamia vyombo vya habari.

Sungura alifika kwenye kiwanja cha Baraza kilichopo Bagamoyo eneo la Kimalang'ombe lenye viwanja 19 na kulikagua pamoja na miundombinu inayozunguka eneo hilo ili kuona namna gani ya kufanya uendelezaji kwa siku za usoni.

Kiongozi huyo wa Baraza pia alilitembelea shamba lenye ukubwa wa ekari 13.8 lililopo eneo la Zinga, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani na kujionea shughuli zinazoendelea katika mali hizo za Baraza.

Ziara hii ilifanyika siku chache tangu akabidhiwe ofisi na mtangulizi wake Kajubi Mukajanga, Januari 16, 2024.

Pia Katibu Mtendaji huyo alitembelea ofisi ya MCT Zanzibar ili kujionea shughuli zinazofanywa na ofisi hiyo pamoja na kukutana na wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kueleza mipango yake.

Wakati huo huo, Februari 08 2024, Katibu Mtendaji alimtembelea mjumbe wa Bodi ya Wadhamini Jaji mstaafu Joseph Warioba nyumbani kwake, kama sehemu ya kujitambulisha na kumweleza mipango yake ya kuliendeleza Baraza.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa ziara za Katibu Mtendaji, wa kujitambulisha kwa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), ambapo amewatembelea Profesa Geoffrey Mmari na Jaji Augusta Bubeshi.





*Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura akionyeshwa mipaka ya shamba la MCT na mfanyakazi wa shamba hilo, Rajabu Ibrahimu Februari 8, 2024. Shamba hilo lenye ukubwa wa ekari 13.8, lipo eneo la Zinga Wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani. Picha ya juu mfanyakazi mwingine wa Baraza Kassim Mbagala akimpa maeleze kuhusu viwanja wa Baraza katika eneo la Kimalang'ombe.*

# Sungura ahimiza mwelekeo mpya wa mabadiliko MCT

Na Mwandishi wa Barazani

Uongozi mpya wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) umekuja na mtazamo mpya wa mabadiliko kushughulikia kitofauti masuala ya matatizo ya vyombo vya habari ili kupata matokeo kwa ufanisi kwa njia za ushirikiano.

Akizungumza katika mahojiano yaliyochapishwa katika jarida dada la Media Watch, Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura, amesema kuwa uongozi mpya siyo Katibu Mtendaji pekee bali hata Bodi nayo ni mpya , ilichaguliwa Septemba mwaka jana.

Katika kipindi cha miezi sita kilichopita uongozi huo mpya umekuwa ukichanganua kwa ndani na pia kushirikiana na wadau wengine wa nje wakiwamo washirika wa maendeleo.

Sungura amesema" ingawa kazi inaendelea, tumebuni nadharia ya mabadiliko kuboresha sekta ya habari kwa kushughulikia masuala ya ndani ya Baraza, taasisi za habari, vyombo vya habari, serikali na washirika wengine".

Tayari, amesema Sungura kuwa uongozi mpya umeanza kutekeleza kwa vitendo nadharia hiyo ya mabadiliko.

Kwa kuwa taifa litafanya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwaka 2024 na 2025, Baraza kwa kutumia timu ya wanahabari na wataalamu wa maendeleo limekamilisha nadharia ya uchaguzi ya mabadiliko.

Nadharia hiyo inaeleza kuwa ' baadhi ya wanasiasa na vyama vya siasa wanatoa ahadi zisizo na tija kwa wapiga kura wakati wa uchaguzi. Ili kuwawajibisha, watanzania wanahitaji kuwezeshwa kufanya maamuzi sahihi ya uchaguzi katika sanduku la kura.Hii inawezekana ikiwa uwezo wa vyombo vya habari vya Tanzania utaimarishwa kupitia wanahabari na wahariri wachache watakaokuwa wakifanyakazi huru bila kuingiliwa na wanasiasa na vyama kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Nadharia hiyo ya mabadiliko imeandaliwa kukuza umahiri wa waandishi wa habari kwa kuimarisha ufuatiliaji wa uchaguzi wa vyombo vya habari kwa lengo la kuwawajibisha wanasiasa na vyama vya siasa kutokana na ahadi zao za wakati wa kampeni za uchaguzi.

Hii itasaidia kwa muda mrefu kuwezesha Baraza kuchangia kwa kuwa na Tanzania yenye jamii ya demokrasi zaidi. Hivi ndivyo Baraza lilivyoona miaka 30 iliyopita, alisema Sungura.

Amesema kuwa Baraza chini ya uongozi mpya linalenga kupata matokeo muhimu mawili ambayo kwanza ni kuwa na mazingira wezeshi ya kihabari na kisheria kuhakikisha uhuru wa habari, usalama wa wanahabari,uhuru wa uhariri na kujisimamia na pili , kukuza weledi wa uandishi kwa viwango vya juu na uwajibikaji.

Kwa kufanikisha masuala ya mabadiliko , Baraza liliandaa mafunzo kwa watendaji wake kuhusu masuala ya mabadiliko na kupanga upya uongozi wa Baraza .

Juhudi kubwa zinafanywa kutafuta raslimali fedha kuwezesha Baraza kujiendesha kwa kuwa wafadhili wengi hawatoi mchango kugharimia Baraza kwa asilimia 100.

Kuhusu kushirikiana na taasisi zingine za kihabari, Sungura alisema hilo ni jambo muhimu kwani umoja ni nguvu.

Alisema Baraza linahitaji kuratibu kwa ufanisi na



Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura.




Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura (kushoto) akimkabidhi fomu ya kujiunga na uanachama wa Baraza hilo meneja wa Radio ya Jembe FM, Albert George Sengo (katikati), mnamo Juni 08, 2024 wakati alipowatembelea kwenye ofisi zao zilizopo Kirumba jijini Mwanza. Kulia ni Gloria Kiwia ambae ni Mhariri Mkuu katika kituo hicho.

kwa wakati jitihada za pamoja za wadau na makundi kuwezesha kuwa na mazingira mazuri ya mfumo huru wa habari nchini kwa ajili ya Tanzania ya kidemokrasia yenye vyombo huru vya habari vinavyowajibika.

Katika mahojiano hayo, Katibu Mtendaji Sungura pia alizungumzia suala Baraza Huru ya Habari ya Serikali ambapo alisema uongozi mpya wa MCT utafanyakazi kujijengea uhalali na heshima mbele ya umma na kutimiza majukumu yake kwa uhuru kusimamia viwango vya weledi vya uandishi wa habari na kujenga mazingira bora ya habari nchini.

Kwa mtazamo wetu itakuwa kwa umma wenyewe kuamua kutumikiwa na chombo chetu cha kujisimamia wenyewe au cha kiserikali.

Alisema kwa sasa , wadau wa habari wanahitaji kuangalia upya hiyo inayoitwa Baraza Huru la habari kama kweli ni huru na kwamba serikali haina kura ya turufu kwa kuanzisha baraza hilo na kama wajumbe wake watakuwa huru na kama muundo wao unahakikisha uhuru wa habari, uhuru wa uhariri na usalama wa waandishi.

Uongozi mpya wa Baraza alisema unafahamu yaliyomo katika suala hilo. Majadiliano zaidi na mashauriano miongoni mwa wadau wa habari na serikali ni muhimu yaendelee kupata ufumbuzi na kuangalia umuhimu wa Baraza la habari la kujisimamia lililoanzishwa na wadau wa habari miaka30 iliyopita.

# Vyuo vyahimizwa kuzingatia ubora taaluma

*Inatoka Ukurasa wa 9*

Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kushirikiana ili kunusuru hali hiyo.

Kwa upande wa walimu wanaotumikia vyuo vikuu, Mwaffisi alisema vyuo hivyo vinapaswa kuangalia kama inafaa kusajili wahitimu walio na alama za juu za masomo na kuwabakisha kwa nafasi za ualimu bila kuzingatia uzoefu wao wa tasnia.

“Wengi wa walimu hawa hawajawahi kupita kwenye vyumba vya habari na hata wengi wao hawajawahi kuandika lakini huko vyuoni wanafundisha namna ya kuandika habari. Hii ni hatari sana kwa tasnia” alisisitiza Dk. Mwaffisi

Dk. Mwaffisi pia alidokeza changamoto nyingine ni kuwa kumekuwa na kukosekana kwa nia ya kweli miongoni mwa baadhi ya wanafunzi wanaosoma au kujishughulisha na uandishi wa habari.

"Wanafunzi wengi hujiandikisha katika kozi za uandishi wa habari si kwa mapenzi ya fani hiyo bali kutokana na shinikizo za nje au kutaka umaarufu kwenye televisheni na redio," alibainisha.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Ernest Sungura alisema kuwa dhamira ya Baraza hilo kama chombo huru cha wadau kilichoundwa kwa lengo la kujisimamia, ni kuhakikisha kinasimamia maadili, kukuza uhuru wa vyombo vya habari na kudumisha viwango vya juu vya taaluma na uwajibikaji.

Sungura aliangazia changamoto zinazoendelea kuvikabili vyombo vya habari nchini Tanzania, kama vile sheria zinazozuia uhuru wa kujieleza, akitoa mfano wa baadhi ya vifungu vya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016.

Uzinduzi wa ripoti hiyo umetoa hali halisi ya tasnia ya habari nchini na hivyo kuwafanya wadau wa habari kujitathmini na kuangalia ni namna gani wataweza kurekebisha baadhi ya changamoto zilizotajwa katika ripoti hiyo ili kuwa na waandishi wenye weledi na kuzingatia maadili na mwisho wa siku kuwa na tasnia imara kwa mustakabali wa taifa.



*Baadhi ya waalikwa katika uzinduzi wa Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari.*

# Samia awapongeza wanahabari wanne kwa kuliheshimisha taifa

Na Mwandishi wa Barazani

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amewapongeza wanahabari wanne kwa kupata tuzo na kuteuliwa kuongoza vyama vya habari Afrika.

Beatrice Bandawe Mhariri Mtendaji wa Nipashe hivi karibuni alitambuliwa na kutuzwa kama kiongozi mwanamke na Chama cha Kimataifa cha Wachapishaji Habari ambapo Rais Samia alisema "hii ni mara ya kwanza kwa mtanzania kupewa tuzo hiyo na tunashukuru".

Ernest Sungura,Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) amekuwa mwenyekiti wa kwanza wa Umoja wa Mtandao wa Mabaraza Huru ya Afrika (NIMCA).

Alichaguliwa kushika wadhifa huo katika mkutano wa wakuu Mabaraza ya Habari Afrika uliofanyika Cape Town, Afrika Kusini. NIMCA ilizinduliwa rasmi Mei 16, 2024, katika mkutano wa kwanza wa Mabaraza ya Habari ya Afrika mjini Cape Town.

Mwenyekiti wa Jukwaa laWahariri Tanzania (TEF) Deodatus Balile alichaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Wahariri cha Afrika Mashariki kwa mwaka 2024/2025 wakati Kajubi Mukajanga amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Mabaraza ya Habari ya Afrika Mashariki.

Rais aliwapongeza wote kwa kuheshimisha taifa katika hotuba yake ya ufunguzi wa Kongamano la pili la kitaifa la Maendeleo ya Sekta ya habari lililofanyika Dar es Salaam Juni 18 na 19, 2024.

Kongamano hilo liliandaliwa kwa pamoja na Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CoRI) na Wizara Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya habari.



*Beatrice Bandawe, Mhariri Mtendaji Nipashe*



*Ernest Sungura, Katibu Mtendaji Baraza la Habari Tanzania (MCT)*



*Deodatus Balile, Mwenyekiti Jukwaa la Wahariri (TEF)*



*Kajubi Mukajanga, Mwenyekiti Baraza la Habari Afrika Mashariki.*



*Kikao cha Bunge kikiendelea.*

# Wadau waridhishwa na Bajeti ya Wizara ya Habari

**Na Saumu Mwalimu**

Aliyekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye amesema Wizara imejipanga kuhakikisha mapinduzi ya kidigitali yanawezeshwa na TEHAMA na kuimarishwa kwa mfumo wa upashanaji habari kwa kusimamia uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Ameongeza kuwa Wizara pia imejipanga kukamilisha maboresho ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, na kutengeneza mkakati wa ulinzi wa watoto dhidi ya ukatili mtandaoni.

Nape aliyasema hayo Mei 16, 2024 wakati akiwasilisha bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambapo jumla ya sh. bilioni181 zimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida ya Wizara hiyo kwa mwaka 2024/2025.

Wadau wa habari likiwemo Baraza la Habari Tanzania (MCT), ambalo liliwakilishwa na Kaimu Meneja Programu, Saumu Mwalimu, wameshuhudia kuwasilishwa Bungeni kwa Bajeti hiyo ambayo imekonga nyoyo za wadau wa habari nchini.

Wadau wengine waliohudhuria shughuli za usomwaji wa Bajeti hiyo ni pamoja na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), JamiiForums, Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), vyombo vya habari na waandishi wa habari.

Baada ya kusomwa kwa Bajeti hiyo, wadau wa habari walikuwa na maoni yafuatayo juu ya bajeti hiyo. Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Kenneth Simbaya alisema bajeti ya mwaka huu ni nzuri inayotia matumaini ukiangalia pamoja na mipango iliyowekwa.

“Ukilinganisha na bajeti zilizopita, kuna mambo unayaona ni ya tofauti katika bajeti hii, japokuwa bado yapo yale ambayo yameendelea kuwepo katika kila bajeti, ninaamini, kama mipango iliyowekwa itatekelezwa itasaidia kuiboresha sekta ya habari.

“Waziri amekuwa akirudia mara kwa mara kwamba waandishi wa habari chini ya Rais Samia Suluhu Hassan wapo salama, tusingependa usalama huo uwe ni utashi wa kiongozi, bali mifumo inayowekwa ambayo hata akija kiongozi mwingine, waandishi waendelee kuwa salama,” alisema.

Simbaya alisisitiza kwamba Wizara iendelee kuitazama sekta binafsi zikiwemo asasi kama mdau muhimu katika kutimiza malengo ya Wizara yake.

“Na nitoe wito kwetu sisi wadau, pale tunapoona tunaweza kuisaidia serikali iwe kwa mali ama mawazo tufanye hivyo, kwa sababu mafanikio hayaletwi na mtu au taasisi moja,” aliongeza Simbaya.

Naye mwandishi wa habari na mtangazaji mkongwe, Rose Haji alisema katika historia yake ya kufuatilia bajeti, hii ndio bajeti ya kwanza ambayo imetambua umuhimu wa vyombo vya habari, mwandishi wa habari na habari katika nchi.

Alisema kwamba kwa Wizara na hata wabunge kujadili kuona namna gani inaweza kujipanga na kuweka kiasi cha fedha kwa ajili ya wanahabari, inaonyesha ukuaji wa thamani wa kada hiyo.

“Tumeshuhudia Bunge likitoa umuhimu kwa habari, vyombo vya habari na hata mwandishi, wabunge wamejadili kuhusu suala ya uchumi wa vyombo vya habari kwa mfano, yamejitokeza mapendekezo kadhaa wakitaka Wizara kuweka angalau asilimia fulani ya bajeti yake kwa ajili ya maendeleo ya vyombo vya habari sambamba na kuhakikisha Wizara hiyo inasimamia ulipwaji wa madeni ambayo yamekuwepo kwa zaidi ya miaka saba,” alisema Bi. Haji.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa

Endelea Ukurasa wa 18

# Samia aombwa kuwa mgeni rasmi mkutano wa kimataifa wa wanahabari

Na Mwandishi wa Barazani

Mwenyekiti wa Jukwaa jipya la Mabaraza Huru ya Habari ya Afrika - Umoja wa Mabaraza Huru ya Habari Afrika (NIMCA) – Ernest Sungura amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan awe mgeni rasmi wa mkutano wa kimataifa wa wadau wa habari unaotarajiwa kufanyika nchini mwakani.

Sungura ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa (CoRI) amesema kwa kupitia mabaraza huru ya habari mwakani" tumepanga kuwaleta Tanzania wadau wa habari kutoka Afrika na Duniani".

Akizungumza mbele ya Rais Samia wakati wa Kongamano la pili la Kitaifa la Maendeleo ya Sekta ya Habari nchini kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam, Sungura alisema hii si tu kwa sababu ya heshima waliyotupatia Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla bali imekuwa ndoto ya serikali yako kuwa na chombo cha kuunganisha waandishi wa habari ambacho kitaweka habari chanya za bara hili kama ulivyosema katika hotuba yako wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari Duniani yaliyofanyika Arusha mwaka 2022. Maadhimisho hayo ya Arusha yalihudhuriwa na wawakilishi wa nchi na mashirika mbalimbali ya Afrika.

Kongamano la pili la kitaifa lililoandaliwa kwa ushirikiano kati ya CoRI na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 1,000 wakiwemo waandishi,maofisa mawasiliano wa serikali na wadau. Rais Samia alikuwa mgeni rasmi.

Maandalizi ya mkutano huo mkubwa wa wanahabari wa Afrika yameanza na " lengo letu ni kufanikisha heshima tuliyopewa na Afrika na duniani kwa jumla", alisema Sungura.

Sungura alichaguliwa mwenyekiti wa kwanza wa NIMCA ilipozinduliwa Mei 16, 2024 katika mkutano wa kwanza wa Mabaraza ya Habari ya Afrika ulioitishwa na Baraza la Habari la Afrika Kusini, mjini Cape Town.

Latiefa Mobara wa Baraza la Habari la Afrika Kusini; George Sarpong wa Tume ya Kitaifa ya Habari ya Ghana, akiwakilisha Afrika Magharibi; na Kennedy Mambwe wa Baraza la Habari la Zambia akiwakilisha Kusini mwa Afrika wanaunda bodi ya awali ya utendaji ya NIMCA wakiweka msingi wa chombo hicho.

Sungura, akiwa mwenyekiti wa kwanza wa NIMCA, alieleza kufurahishwa kwake kwa jukumu hilo jipya kwa kusema " hii ni siku muhimu kwa sekta yetu ya habari. Mabaraza yetu ya habari kwa muda mrefu yamekuwa yakifanyakazi kipekee pekee na yamekuwa na ushirikiano mdogo wa kubadilishana taarifa. NIMCA inaanzisha zama mpya ya kuhimiza ushirikiano, kuimarisha uhuru wa habari, mifumo ya uwajibikaji na kuhamasisha uandishi mahiri, makini na wa heshima katika bara letu."

Mkutano huo wa Cape Town ulihudhuriwa na washiriki mbalimbali wakiwemo wa kutoka mabaraza huru na kiserikali.

Washiriki walibadilishana uzoefu na changamoto za uhuru wa habari na walijadili kuwa na mazingira ya kuzingatia maadili ya habari ambapo vyombo vya habari na vyombo vya usimamizi vinakabiliwa na matatizo ya fedha na uendelevu.

NIMCA inakaribisha wasimamizi huru kutoka nchi zingine za Afrika kujiunga na umoja huo kuhimiza kujisimamia kama msingi na nguzo ya huru na weledi wa vyombo vya habari katika maendeleo na mabadiliko ya uwanda wa mawasiliano. Hii ni muhimu hasa ambapo habari za mtandaoni zinahusishwa zaidi na kusambaza maudhui ya kinyume cha maadili na kiwango cha chini cha uandishi wa habari.

Mabaraza hayo yamewataka waandishi wa habari, wapiga picha na watendaji wengine wa habari kuzingatia misingi ya uandishi ili kuzuia usimamizi wa serikali na hatua kali za wenye mamlaka. Wamekiri kuwepo haja ya kutafuta na kukuza aina mpya ya kupata misaada ya fedha kuendeleza na kukuza uandishi na mifumo ya kujisimamia katika tasnia hiyo.

Katika mabadiliko ya kasi ya mazingira ya kidijiti, vyombo vya kusimamia habari vimeona kuna umuhimu wa miongozo ya jinsi vyombo vya habari vinaweza kuangalia masuala ya maadili kufuatia kuibuka kwa akili mnemba (AI) na haja ya kuwa na ubunifu katika mitaala ya uandishi wa habari na miundo ya utoaji mafunzo.

# TEF yalaani kushambuliwa mwandishi

Na Mwandishi wa Barazani

Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) limesikitishwa na kulaani kitendo cha kushambuliwa kwa mwandishi wa habari wa kampuni ya The Guardian, Dickson Ng'hily, kilichofanywa na walimu wa Shule ya Msingi Kwembe Wilayani Ubungo, Dar es Salaam, wakati akitekeleza majukumu yake.

Katika taarifa yake dhidi ya shambulio hilo lilitokea Julai 10, 2024 kwa madai kuwa amewapiga picha wanafunzi wa shule hiyo wakisoma nje ya madarasa chini ya mti, TEF imelielezea tukio hilo kuwa ni jinai.

Baada ya kumshambulia, walimu walikwenda mbali zaidi kwa kumpeleka mwandishi huyo katika ofisi za Serikali ya Mtaa na baadaye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo.

Licha ya kipigo, walimu hao na wanafunzi waliharibu vifaa vyake vya kazi ikiwamo simu ya mkononi waliyoipasua kioo, wakamnyang'anya na kufuta picha alizopiga.

TEF imeeleza katika taarifa hiyo ya Julai 12, 2024 kuwa ni muhimu ifahamike kuwa uandishi wa habari chini ya Kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Huduma za Habari (MSA) ya Mwaka 2016 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2023, ni taaluma inayotambulika kama taaluma nyingine nchini.

Jukwaa hilo limesema kuwa hatua ya kumweka chini ya ulinzi kujiridhisha kama ana kibali cha kupiga picha ni mwendelezo wa jinai sawa na walivyofanya walimu waliompiga Ng'hily.

"Tunajiuliza ukaguzi huo walitaka kuufanya kwa kutumia sheria ipi au walipata wapi mamlaka hayo? Nani kawaambia mwandishi wa habari akikuta tukio linaendelea anapaswa kuandika barua ya maombi ya kibali cha kupiga picha, kiidhinishwe kwanza ndipo arudi kupiga picha?

"Hivi hilo tukio atalikuta likiendelea akifuata utaratibu huo? Duniani kote, mwandishi akikuta tukio anapiga picha kwanza kisha anawatafuta wahusika kupata ufafanuzi,"TEF imeeleza na kuhoji kwa nini Wilaya ya Ubungo na Walimu wa Shule ya Msingi Kwembe wanataka kutunga kanuni mpya isiyokidhi vigezo vya uandishi wa habari?

" Kitendo kilichofanywa na walimu hao ni jinai na hujuma dhidi ya juhudi anazofanya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kurejesha uhuru wa vyombo vya habari nchini kwa kuzuia waandishi kukamatwa, kupigwa, kuzuiwa kufanya kazi, kunyanyaswa na mengi ya aina hiyo ambayo ameyazuia tangu alipoingia madarakani Machi 19, 2021 hali iliyoipandisha Tanzania katika viwango ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kwa nafasi 46, yaani kutoka nafasi ya 143 hadi nafasi ya 97," imeeleza taarifa hiyo ya TEF iliyotiwa saini na Mwenyekiti wake, Deodatus Balile.

TEF imesisitiza "vitendo vya aina hii vikiendelea nchi yetu itashuka tena na kuathiri kuaminika kwake mbele ya jamii ya kimataifa hivyo kukimbiza wawekezaji."

TEF imelaani kwa nguvu zote kitendo hiki na kuvisihi vyombo vya dola vimpe ushirikiano wa kutosha Mwandishi Ng'hily, ambaye tayari ameanza mchakato wa kufungua kesi ya jinai dhidi ya wote waliohusika katika kadhia hii.

Jukwaa hilo limesisistiza litamuunga mkono mwandishi huyo hatua kwa hatua kuhakikisha wahusika wanachukuliwa h atua stahiki ikiwa ni pamoja n a kulipa gharama ya hasara waliyoisababisha na iwe fundisho kwa wengine waache kujichukulia sheria mkononi.

Katika hatua nyingine TEF imeeleza inafuatilia kwa karibu tabia iliyoibuka hivi sasa ya baadhi ya watu kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu kuuawa au kutekwa kwa watoto katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika taarifa yake iliyosainiwa na Mwenyekiti wake Balile TEF imeeleza yamekuwapo matukio kadhaa ya taarifa za aina hii katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, huko Kigamboni, Mbagala na Kipawa, ambayo yameleta taharuki kubwa hadi wazazi wakafuata watoto shule, lakini baadaye ikathibitika kuwa siyo kweli.

"Tabia hii ya kupokea na kusambaza taarifa ambazo hazina uhakika au ukweli, husababisha taharuki, usumbufu, na mshtuko kwa wazazi, walezi, watoto, na wananchi kwa ujumla.

TEF inawaomba Watanzania kutoa taarifa ambazo wana uhakika nazo ili kuepuka kusababisha taharuki na hofu kubwa.Tunaomba wananchi wasisambaze taarifa ambazo hawana uhakika nazo au kufahamu undani wa ukweli wake, kwani ni kosa la jinai kisheria na siyo maadili ya uandishi wa habari kuisumbua jamii",tamko hilo limesema

TEF imetoa mwito kwa wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa kuwatunza na kuwalinda watoto wao na imewasihi Polisi na kuwataja kuchunguza matukio yanayotajwa, na waongeze ulinzi katika maeneo mbalimbali nchini ili kuendelea kuaminika kwa wananchi na wajione wako salama.

# Wadau waridhishwa na Bajeti ya Wizara ya Habari

*Inatoka Ukurasa wa 16*

JOWUTA, Selemani Msuya, alisema hotuba imeonyesha mwelekezo mzuri na kushauri kuwepo kwa mifumo ya kisheria itakayolinda sekta hiyo na sio kutegemea hisani ya kiongozi aliyepo madarakani.

"Waziri ameeleza walivyojipanga kutatua changamoto za sekta ya habari ikiwemo kulipa madeni na waandishi wa habari kupata mikataba ya ajira hilo haliwezi kufanyika kwa kuamini utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan pekee, bali mifumo inatakiwa kupewa nafasi," alisema.

Aidha amezishauri taasisi za kihabari kushirikiana katika kupigania maslahi ya waandishi wa habari ambao wengi wanapitia wakati mgumu kichumi, kijamii na kikazi.

Akizungumzia suala la uhuru wa kujieleza kama lilivyotajwa kwenye bajeti ya Wizara, Mkurugenzi Mtendaji wa JamiiForums Maxence Mello amesema Serikali imefurahishwa na ripoti ya Reporters Without Boarders, kwa sababu tumepanda viwango, lakini tumepanda kwa utaratibu gani.

"Tanzania iliwahi kuwa nafasi ya juu zaidi ya 97, nadhani tuliwahi kuwa ya 65 miaka ya nyuma, sasa tumefikaje hadi 143 hadi tuishangilie hii ya 97 ni kwamba hatusikilizani, ni kama tunagombea fito wakati tunajenga nyumba moja" alisema.

Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya wadau wa ndani ya sekta ya umma, asasi za kiraia na sekta binafsi katika kujenga uwanja mpana na kuilinda Ibara ya 18 na kuhakikisha uhuru wa kujieleza unadumishwa, vyombo vya habari vinalindwa, kwa mujibu wa sheria na taratibu tulizojiwekea na sio tulizowekewa.

# Uandishi wa habari ni taaluma sio *Smartphone*



Na Tumbi Kiganja

Mitandao ya kijamii imekuwa ni chachu kubwa sana katika sekta ya mawasiliano hasa kwa uwezo wake wa kupasha habari kwa haraka pindi tu tukio linapotokea, huku ikiruhusu mijadala ya moja kwa moja kwa njia za maongezi na maandishi. Hii inaifanya mitandao hii kuwa tofauti kidogo na vyombo vya habari asilia kwa maana ya runinga, redio na magazeti.

Tangu mabadiliko makubwa ya kitekinolojia yaingie nchini, na kuruhusu uwepo wa mitandao hii ya kijamii kama X zamani Twitter, WhatsApp, Instagram, Facebook, Tiktok, Youtube, Tinder, Threads na mingineyo, kumekuwa na faida kadhaa ikiwemo utafutaji na upatikanaji wa taarifa kwa haraka, kuunganisha marafiki mbalimbali waliopotezana miaka mingi, uundwaji wa makundi sogozi (WhatsApp groups) ya kikazi, familia nakadhalika.

Ingawa mitandao hii pia imekuja na changamoto zake kwa baadhi ya watumiaji (Jamii) hasa wale wasiojua nguvu na athari za mitandao hiyo na kujikuta wakichapisha taarifa au picha zisizo sahihi zilizojaa upotoshaji. Hali hii huchangiwa na kutojua matumizi sahihi ya mitandao hiyo.

Kawaida, mwenye akaunti ya mtandao wa kijamii yeye ndie mmiliki wa akaunti hiyo ambayo kwa mujibu nwa sheria ni lazima iwe na nywila (password). Hivyo yeye pia ndio mdhibiti maudhui katika akaunti yake.

Hali hii inafanya kila mmoja mwenye akaunti kuandika au kupiga picha tukio lolote analoliona mbele yake bila kujali au kuzingatia suala la maadili juu ya picha au habari aliyochapisha.

Mara kadhaa kumeshuhudiwa taarifa/habari za upotoshaji kuhusu vifo vya watu maarufu au taarifa zenye maslahi ya kitaifa zikisambazwa kwenye mitandao ya kijamii ingawa baadae wenyewe (waliozushiwa) hujitokeza na kukanusha na kisha kukemea vikali juu ya upotoshaji huo.

Mitandao hii pia imekuwa ikidhalilisha baadhi ya makundi katika Jamii. Kwa mfano, kumekuwa na matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto hasa wale waliokumbatana na ukatili wa kijinsia kama ulawiti. Baadhi ya kurasa za mitandao ya kijamii imekuwa ikichapisha picha ama video zao, majina yao na ndugu au wazazi, umri wao na kadhalika.

Hii ni kinyume na kanuni za maadili ya uandishi wa habari pamoja na miongozo yake ukiwemo ule wa MCT kuandika habari za watoto unaowataka waandishi kutochapisha picha au video za watoto ambao ni waathirika wa matukio ya udhalilishaji

Aidha, katika ufuatiliaji wa mienendo ya vyombo vya habari nchi, ripoti ya MCT inaonyesha kuwa tangu Januari hadi Julai 5, 2024 jumla ya matukio 10 yamekusanywa. Matukio haya ni yale yanayohusu vyombo vya habari kuchapishwa bayana taarifa za watoto ambao ni waathirika wa matukio ya udhalilishaji wa kingono.

Katika matukio hayo kumi, saba ambayo ni asilimia sabini yalitoka kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni. Katika mikutano ya kutatua kero za wananchi wa Jiji la Arusha inayofanwa na Mkuu wa Mkoa huo Paul Makonda, kumekuwa na uvunjifu wa maadili ya kiuandishi kwa vyombo vingi vya mtandaoni.

Kwa mfano, baadhi ya watu akina mama/watoto wanaokwenda mbele ya Mkuu wa Mkoa kuomba msaada ni wale waliopitia udhalilishaji. Baadhi ya vyombo hivi vimekuwa vikiwaonyesha bayana bila kuficha utambulisho wao.

Pamoja na changamoto hizi, MCT bado imekuwa ikifanya jitihada ya kutoa mafunzo ya namna ya kuchapisha habari kwa kuzingatia maadili kuwasiliana moja kwa moja na wahariri wa vyombo husika na kuwajulisha juu ya makosa ambayo wamefanya kwa habari husika, ingawa bado baadhi ya vyombo vimekuwa vikirejea makosa ya namna hii.

Ikumbukwe kuwa, MCT ni chombo kilichoundwa na wadau wa tasnia ya habari nchini kwa lengo la kusimamia na kukuza maadili na weledi katika taaluma ya uandishi wa habari nchini. Hivyo haina mamlaka na wala si lengo la kuanzishwa kwake kuwaadhibu au kutoa adhabu kwa wale wanaofanya makosa ya kitaaluma. Imeendelea kuwa kama kiranja anaewakumbusha wenzake wasipige kelele kwani mwalimu (mamlaka) inaweza kuja kuwawajibisha.

Baadhi ya vyombo vya habari vya mtandaoni au watu binafsi mara kadhaa wamejikuta matatani na kuangukia mkono wa sheria kwa kushtakiwa kwa kutumia Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA)

Hii ni moja ya sheria zinazobinya uhuru wa habari na ule wa kujieleza ambapo wadau mbalimbali ikiwemo MCT wameendelea kushirikiana wakitaka mabadiliko yafanyike kwa baadhi ya vifungu ambavyo vinaonekana kubinya uhuru huo.

Ni vizuri watumiaji wa mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari vya mtandaoni kufahamu kuwa sheria hii bado ipo na inafanya kazi hivyo ni vizuri kuchagua nini cha kuchapishwa na nini cha kuacha. Kwa upande wa vyombo vya mtandaoni viendelee kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya kitaaluma.

Jamii pia inapaswa kujua kuwa uandishi wa habari ni taaluma yenye misingi na miiko yake, hivyo si kila kinachochapishwa mitandaoni basi ni habari. Aidha, kumiliki simu ya kisasa yenye uwezo wa kupiga picha haikupi ithibati ya wewe kuwa mwandishi wa habari.

# SMZ yaombwa kupitisha Sera na Sheria za Habari

**Na Mwandishi wa Barazani**

Baraza la Habari Tanzania (MCT), limeiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa majadiliano ya kutaka mabadiliko ya Sera na Sheria za Habari Zanzibar yahitimishwe kwa wadau kupata sera na sheria nzuri.

Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura ameyasema hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari yaliyofanyika katika ukumbi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), mjini Zanzibar Mei 23, 2024.

"Tunaiomba serikali kufanya mabadiliko ya Sheria na Sera za Habari Zanzibar na majadiliano ya kutaka mabadiliko haya yawe ya mwisho tupate sheria na sera nzuri, tunataka kuona vitendo maana muungwana ni kitendo," alisema Sungura.

Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni "Uhuru wa Vyombo vya Habari na Mageuzi ya Sera na Sheria za Habari Zanzibar".

Naye Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi Habari Zanzibar (ZPC), Abdallah Mfaume alisema kauli mbiu ya kitaifa imejikita katika suala la mazingira, lakini ili kujikita katika uandishi wa Habari mahususi, tunahitaji sheria na sera ambazo zitawahakikishia waandishi wa habari uhuru na usalama wao.

"Kauli mbiu ya Kitaifa imejikita katika mazingira lakini tunahitaji sheria na sera ambazo zinaweza kutuhakikishia uhuru wetu na usalama wetu ili tuweze kufanya kazi ya uandishi kwa weledi", alisisitiza Mwenyekiti wa ZPC.

Akizungumza katika Kongamano hilo, Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdalla alisema Serikali imekusudia kuvizawadia vyombo vya habari ambavyo vimefanya vizuri kwa mwaka mzima bila kukinzana na sheria, pamoja na kuanza kutoa udhamini kwa makongamano ya aina hii.

Aliwataka waandishi wa habari kujikita zaidi kwenye uandishi wa habari unaozingatia maadili na taaluma ya habari, na kuwataka kuacha uandishi wa habari wa mihemuko.

Maadhimisho ya siku ya uhuru wa Habari yameratibiwa kwa ushirikiano wa MCT, Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Chama cha Waandishi Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA) na Wakfu wa Jumuiya ya Madola.




*Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi Zanzibar (ZPC), Abdallah Mfaume akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari Duniani.*